**BENKI KUU YA TANZANIA**
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Simu: +255 22 223 3167
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz

**BANK OF TANZANIA**
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Phone: +255 22 223 3167
Email: botcommunications@bot.go.tz

**4 Aprili 2024**

# Taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha

**Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) imepandisha Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate-CBR) kutoka asilimia 5.5 iliyotumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 hadi asilimia 6, ambayo itatumika katika robo ya pili ya mwaka 2024, yaani mwezi Aprili hadi Juni 2024.** Uamuzi huo ulifikiwa katika kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika tarehe 3 Aprili 2024 na umezingatia tathmini ya mwelekeo wa uchumi iiliyofanyika mwezi Machi 2024. Kamati imeona umuhimu wa kuongeza Riba ya Benki Kuu hadi asilimia 6, itakayokuwa na wigo wa asilimia 2 juu na chini, ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei siku zijazo kutokana na athari za mwenendo wa uchumi wa dunia.

Kutokana na tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia, Kamati imebaini kuwa, katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, ukuaji wa uchumi uliimarika katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua, sambamba na kuimarika kwa ukwasi katika masoko ya fedha. Bei za bidhaa katika soko la dunia imebaki tulivu. Mathalan, bei ya mafuta ghafi ilikuwa wastani wa dola 80 kwa pipa, wakati bei ya dhahabu imeendelea kubaki juu, ikiuzwa kwa wastani wa dola za Marekani 2,071 kwa wakia moja. Hali hii inatarajiwa kuendelea katika kipindi kijacho cha mwaka 2024. Hata hivyo, matarajio haya yanaweza kuathiriwa na uamuzi wa nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi (OPEC+) kuhusu kiwango cha uzalishaji pamoja na migogoro ya kisiasa inayoendelea.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa Tanzania, Kamati imeridhishwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi, licha ya changamoto zilizotokana na mtikisiko katika uchumi wa dunia. Hali hii ya kuimarika kwa uchumi inatarajiwa kuendelea katika

siku zijazo, hususan robo ya pili ya mwaka 2024. Maeneo mahususi ya mwenendo wa uchumi yaliyofanyiwa tathmini na Kamati ni kama ifuatavyo:

i. Ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuongezeka kufikia asilimia 5.1 kwa mwaka 2023, kutoka asilimia 4.7 mwaka 2022. Aidha, ukuaji wa uchumi unakadiriwa kufikia asilimia 5.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024. Mwenendo huu unatokana na uwekezaji unaofanywa na Serikali hususan katika ujenzi wa miundombinu unaolenga kuongeza uwekezaji kwa sekta binafsi. Vilevile, sekta binafsi imeendelea kuchangia katika kuimarika kwa uchumi kutokana na maboresho yanayoendelea katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Hali hii inadhihirika kutokana na kuendelea kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi na uwekezaji kutoka nje ya nchi.

   Mwenendo wa uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa wa kuridhisha pia, ambapo uchumi umekadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 6 kwa mwaka 2023 kutokana na kuimarika kwa shughuli za uchumi, hususan utalii. Mwenendo huu wa kuridhisha wa ukuaji wa uchumi nchini unatarajiwa kuendelea katika kipindi kijacho cha mwaka 2024. Hali hii inatokana na maboresho yanayoendelea katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, mvua za kutosha katika maeneo mengi nchini, pamoja na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia.

ii. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu, kwa wastani wa asilimia 3.0 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024. Kiwango hiki kilikuwa ndani ya lengo la nchi la mfumuko wa bei usiozidi asilimia 5 na vigezo vya kikanda kwa jumuiya ambazo Tanzania ni mwanachama. Hali hii inatokana na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na uwepo wa chakula cha kutosha nchini. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei umeendelea kupungua kufikia karibu lengo la asilimia 5, kutokana na kupungua kwa bei za chakula na bidhaa zisizo za chakula. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa mdogo na tulivu kutokana na utekelezaji wa sera thabiti ya fedha na upatikanaji wa chakula cha kutosha.

iii. Utekelezaji wa sera ya fedha katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 uliiwezesha riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la jumla la fedha baina ya benki kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3.5 hadi 7.5, kama ilivyotarajiwa. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara, kwa wastani wa takriban asilimia 17. Mikopo hiyo ilielekezwa zaidi katika shughuli za kilimo, uchimbaji wa madini, usafirishaji na uzalishaji viwandani. Mikopo kwa sekta binafsi inatarajiwa kuendelea kuongezeka katika kipindi kijacho cha mwaka 2024 kutokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji.

iv. Utekelezaji wa sera ya bajeti ulikuwa wa kuridhisha, ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 mapato ya Serikali yalikuwa takriban asilimia 95 ya lengo kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya ndani yalivuka lengo kwa asilimia 6.4 kutokana na maboresho katika usimamizi wa kodi na kuongezeka kwa utayari wa wananchi kulipa kodi. Matumizi ya Serikali yameendelea kufanyika kulingana na rasilimali zilizopo, huku deni la Taifa likiendelea kuwa himilivu.

v. Nakisi ya urari wa biashara nje ya nchi iliendelea kupungua kutokana na kupungua kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi. Katika mwaka unaoishia Februari 2024, nakisi ilipungua kufikia dola milioni 2,701.4 kutoka dola milioni 5,133.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kwa upande wa Zanzibar, nakisi ya urari wa biashara pia ilipungua. Nakisi ya urari wa biashara inatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa kwa kipindi kilichobaki cha mwaka 2024.

    Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha, kufikia zaidi ya dola za Marekani bilioni 5.3 mwishoni mwa mwezi Machi 2024, sawa na miezi 4.4 ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa asilimia 1.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.6 katika robo ya mwisho ya mwaka 2023. Hali hii ilitokana na msimu wa mapato madogo ya fedha za kigeni pamoja na mazingira ya kiuchumi duniani.

Kamati pia ilijadili kuhusu changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni nchini na kujiridhisha kwamba hatua za kuongeza upatikanaji na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotekelezwa hivi sasa zinatarajiwa kupunguza changamoto hiyo ndani ya muda mfupi ujao.

vi. Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara na thabiti huku viashiria vyote vya uthabiti vikiwa ndani ya wigo unaokubalika kisheria. Sekta ya kibenki imeendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, huku ikiendelea kutengeneza faida. Ubora wa rasilimali za benki ulikuwa wa kuridhisha, ambapo uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) ulikuwa asilimia 4.3 ambayo iko ndani ya wigo unaokubalika wa uwiano wa chini ya asilimia 5 ya mikopo yote.

**EMMANUEL M. TUTUBA**
**GAVANA**